# ZOEZI LA KUONDOA MIFUGO NA MAKAZI NDANI YA HIFADHI YA SERENGETI NA MPAKA WA PORI TENGEFU LA LOLIONDO

***JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA***

***WIZARA YA MALIASILI NA UTALII***

***TAARIFA KWA UMMA***

***ZOEZI LA KUONDOA MIFUGO NA MAKAZI NDANI YA HIFADHI YA TAIFA SERENGETI NA KWENYE MPAKA WA PORI TENGEFU LOLIONDO***

***Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Ngorongoro, kwa kushirikisha Hifadhi ya Taifa Serengeti na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, inaendesha zoezi la kuondoa mifugo na makazi ndani ya hifadhi ya Taifa Serengeti na kwenye mpaka wa Pori Tengefu Loliondo.***

***Zoezi hilo lililoanza tarehe 10 Agosti 2017 litadumu kwa siku kumi na nne na linashirikisha Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Ngorongoro, Jeshi la Polisi, Usalama wa Taifa, Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, Hifadhi ya Taifa Serengeti na Hifadhi ya eneo la Ngorongoro.***

Search here ... SEARCH

On this Section
» News and Events
» Press Releases
» Tenders and Vacancies
» Campaigns
» Photos
» Videos

News Resources Docs Tags


WAINGEREZA WAVUTIWA KUWEKEZA SELOUS, DK. KIGWANGALLA AAGIZA KUWEKWA MAKUBALIANO YA AWALI (MOU)
May 06, 2018


SERIKALI YAELEZA FURSA ILIYOPO KATIKA UFUGAJI WA NYUKI
May 05, 2018

IDADI YA WATALII NCHINI YAZIDI KUONGEZEKA
May 04, 2018

MAKALA: WIZARA YA MALIASILI NA UTALII INAVYOIMARISHA SEKTA YA UHIFADHI NA UTALII NCHINI
May 03, 2018

Facebook

*Zoezi hilo linalenga kunusuru uhifadhi ndani ya hifadhi, ndani ya Pori Tengefu Loliondo, na ndani ya mfumo ikolojia wa Serengeti na pia kunusuru utalii katika mfumo ikolojia huo.*

*Aidha, hatua hii ya kuondoa makazi na mifugo kutoka katika maeneo ya mipaka ya Pori Tengefu Loliondo kutaongeza uhakika wa kupatikana malisho ya mifugo wakati wa kiangazi kwa kuwa hakutakuwepo na makazi ndani ya Hifadhi na ufugaji holela.*

*kimsingi zoezi hili linaendana na wito wa Serikali wa kuondoa mifugo ndani ya maeneo yote yaliyohifadhiwa nchini.*

*Katika kutekeleza zoezi hili, Mkuu wa Wilaya Ngorongoro, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Ngorongoro Bwana Rashidi Taka, alitoa maelekezo yafuatayo:*

*1. Zoezi litafanyika ndani ya Hifadhi ya Taifa Serengeti na kwenye mpaka wa Pori Tengefu Loliondo. Kwa upande wa mpaka wa Pori Tengefu Loliondo zoezi litaanzia kaskazini hadi kusini urefu wa kilometa 90, na upana wake utakuwa kilometa 5. Kwa ndani ya Hifadhi ya Taifa Serengeti litafanyika upande wa mashariki kuanzia milima ya Kuka (kaskazini) hadi kigingi na. SNP 9 (kusini);*

*2. Maboma yatakayokutwa ndani ya hifadhi yatateketezwa kwa moto na watu watakaokutwa na mifugo watachukuliwa hatua za kisheria, ikiwemo kupelekwa mahakamani;*

*3. Maboma yaliyoko ndani ya mpaka wa Pori Tengefu Loliondo - kwenye mpaka na ndani ya kilometa tano - wataondolewa ili warudi vijijini. Eneo hilo litabaki kwa ajili ya malisho na si kwa ajili ya makazi. Uwepo wa makazi kwenye mpaka wa Hifadhi ya Taifa Serengeti umekuwa kichocheo kikubwa cha mifugo kuingizwa hifadhini.*

*Zoezi hili linalenga kuondoa changamoto kubwa ya mifugo kuingizwa Hifadhi ya Taifa Serengeti na kwenye mpaka wa Pori Tengefu Loliondo, kupambana na uvamizi mkubwa uliofanywa na wahamiaji haramu kutoka nchi jirani na kunusuru vyanzo vya maji kutokana na mifugo kulishwa kwenye vyanzo vya maji na hivyo kusababisha vyanzo hivyo kuharibika na kukosekana kwa maji kwa ajili ya mifugo na wanyamapori.*

Wizara ya Maliasili na …
12,401 likes
Like Page
Share
Be the first of your friends to like this


Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

Simu Na: +255 026 2321566
Nukushi: +255 026 2321514
Barua pepe:

Mtaa wa Kilimani,
Barabara ya Askari,
S.L.P 1351,
40472-DODOMA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Wizara ya Maliasili na Utalii inautaarifu umma kuwa, taarifa iliyotolewa tarehe 09 Mei, 2018 na Taasisi ya Oakland iliyopo nchini Marekani ikiwa na kichwa cha habari **"Losing the Serengeti: the Maasai land that was to run forever"** na kunukuliwa na Shirika la Utangazaji la Uingereza-BBC Swahili kwa kichwa cha habari **"Tanzania yadaiwa kukandamiza haki za Wamaasai wanaoishi Loliondo"** ni potofu.

Taarifa hiyo imeituhumu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa imefanya; uchomaji wa makazi kwa jamii ya wamasai, kuondoa mifugo yao kutoka kwenye maeneo ya malisho na maji, kuwatesa wananchi na kuwazuia kutoa maoni yao, taarifa ambazo si za kweli.

Ukweli ni kuwa, kutokana na umuhimu wa eneo hilo kwa uhifadhi, uwepo wa vyanzo vya maji, eneo la mzunguko wa uhamaji wa wanyamapori na maisha ya watu, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu ilichukua hatua stahiki za kutatua mgogoro huo ikihusisha wadau wote muhimu yakiwemo mashirika yasiyo ya kiserikali, wawekezaji pamoja na wananchi.

Kazi hiyo inaendelea na Serikali itatoa taarifa rasmi kuhusu suala hili.

Wizara ya Maliasili na Utalii inawataka watanzania na jumuiya ya kimataifa kwa ujumla kupuuza taarifa hiyo potofu yenye lengo la kuipaka matope Serikali na kuleta uchonganishi baina yake, wananchi na wawekezaji kwa lengo la kuleta uvunjifu wa amani.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kushirikiana na wadau wenye

***Hadi sasa zoezi hili la kuondoa mifugo na makazi ndani ya Hifadhi ya Taifa Serengeti na kwenye mpaka wa Pori Tengefu Loliondo linaendelea vizuri likihusisha kuchoma moto maboma yote yaliyoachwa na wafugaji walioondoka wakati wa zoezi.***

***Wizara ya Maliasili na Utalii inapenda kuufahamisha umma kuwa hakuna watu wanaopigwa katika zoezi hili.***

***Pia, Wizara ya Maliasili na Utalii inapenda kuutaarifu umma kuwa habari zinazosambazwa mitandaoni ni upotoshaji wa ukweli wenye nia ovu ya kujenga chuki dhidi ya Serikali kwa wananchi wa Loliondo na maeneo yanayopitiwa na zoezi hilo.***

***Aidha, Wizara ya Maliasili na Utalii, inapenda kuweka bayana kuwa, taarifa za kupigwa risasi Pormoson Losso mwenye umri wa miaka 23, mkazi wa Ololosokwan zilitolewa tarehe 8 Agosti 2017 na hazihusiani na zoezi tajwa kwani tukio hilo lilitokea siku tano kabla ya kuanza zoezi la kuondoa mifugo na makazi ndani ya hifadhi wakati zoezi hili lilianza kutekelezwa Jumapili tarehe 13 Agosti 2017.***

***Hata hivyo Serikali inawapongeza wananchi wengi miongoni mwa wafugaji kwa kuunga mkono zoezi hili na kwa ushirikiano wanaotoa.***

***Serikali inatoa onyo kwa yeyote anayejihusisha na upotoshaji wa ukweli kuhusu zoezi hili lenye nia njema linalolenga kunusuru hifadhi, kuacha mara moja ili kujiepusha na hatua za kisheria zitakazochukuliwa pindi atakapobainika.***

***Imetolewa na;***

***Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***

***17/08/2017***

- Twitter Share
- Facebook Share
- Print this Publication
- Recommend to a friend

## ATTRACTIONS

**Tanzania Tourist Attractions**
Tanzania is one of the unique…

**Investments Opportunities**
The Ministry has many potential…

**World Heritage Sites**
Tanzania is a country which…

## USEFUL LINKS

Tanzania Tourist Board

Tanzania National Parks

Tanzania Forest Service (TFS) Agency

Ngorongoro Conserversion Area Authority (NCAA)

## CATEGORIES

| | |
|---|---|
| Budgets | Press Release |
| Policies | Tenders |
| Vacancies | Forms |
| Links | Photos |
| Agencies | Feeback |

## ABOUT US

Ministry of Natural Resources and Tourism of United Republic of Tanzania, is the Ministry responsible for management of Natural, Cultural and Tourism resources. Tanzania has a great potential for natural resources, cultural and tourism attractions. In terms of wildlife, the present…

© 2018 - Ministry of Natural Resources and Tourism Tanzania